**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**KIKAO CHA THELATHINI**

**22 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA THELATHINI - TAREHE 22 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**378 MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kuwalinda Wanafunzi Mashuleni.

**379 MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali haiwaajiri Wahitimu wenye Diploma kuwa Watendaji wa Vijiji.

**380 MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mpalanga - Bahi.

**381 MHESHIMIWA ROSE VICENT BUSIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya Runzewe Mashariki - Bukombe.

**WIZARA YA MAJI:**

**382 MHESHIMIWA MICHAEL CONSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali haioni ni muda muafaka kuchimba visima vya maji kwenye Taasisi za Umma kama Shule, Zahanati na Hospitali zote nchini.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**383 MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Uwanja wa Ndege Mafia utaboreshwa ili Ndege kubwa ziweze kutua.

**384 MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha Meli katika Vijiji vya Nsele na Lifuma ili kuwaondolea adha ya usafiri Wananchi wa maeneo hayo.

**385 MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Taa za kuongozea Ndege zitafungwa katika Uwanja wa Ndege Mpanda.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**386 MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwa nini Askari Polisi hawalipwi fedha za likizo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**387 MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango wa kupima na kupanga makazi yaliyopo kando ya Barabara Kuu ya Moshi - Arusha na Arusha *bypass.*

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **22 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA